HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. *KAPT (MST)* GEORGE H. MKUCHIKA (MB), WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KATIKA UFUNGUZI WA MAFUNZO MAALUM KUHUSU UTEKELEZAJI SAHIHI WA SHERIA, KANUNI, TARATIBU NA MIONGOZO KATIKA UENDESHAJI WA UTUMISHI WA UMMA KWA WAKURUGENZI WA HALMASHAURI NA WAKUU WA IDARA ZA UTAWALA NA RASILIMALIWATU
MOROGORO, TAREHE 01 OKTOBA, 2018

Dkt. Stephen Kebwe, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro;

Bw. Clifford Tandali, Katibu Tawala wa Mkoa wa Mororgoro;

Dkt. Henry Mambo, Mkuu wa Chuo na Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania;

Dkt. Emmanuel Selemani, Mkurugenzi wa Kampasi ya Dar es Salaam;

Bi. Judith Nguli - Mratibu wa Mafunzo – Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania;

Ndugu Waelekezi;

Washiriki wa Mafunzo;

Wanahabari mliopo;

Mabibi na Mabwana;

Habari za Asubuhi.

Ndugu Mkuu wa Chuo, Awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uzima, nguvu na afya njema kwa kutuwezesha kukutana hapa leo katika siku hii muhimu. Pia, nitumie fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa heshima kubwa mliyonipa ya kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika Ufunguzi wa mafunzo Maalum kuhusu "**Utekelezaji Sahihi wa Sheria, Kanuni, Taratibu, na Miongozo katika Uendeshaji wa Utumishi wa Umma Kwa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara za Utawala na Rasilimaliwatu wa Halmashauri zote nchini".**

Ndugu Mkuu wa Chuo,

Naomba nikupongeze wewe binafsi na Menejimenti nzima ya Chuo kwa kazi kubwa na nzuri mnayoifanya ya kujenga uwezo kwa watumishi wa Umma katika Nyanja mbalimbali. Vilevile nampongeza Mkurugenzi wa Kampasi ya Dar es Salaam na timu yake kwa kuratibu mafunzo haya ninayoyafungua leo. Mafunzo haya ni muhimu kwani yana lengo la kuwajengea uwezo Viongozi hawa wa Halmashauri zote nchini, katika namna bora itakayowawezesha kuzifahamu na kuzichambua kwa kina Sheria, Kanuni, miongozo na maboresho mbalimbali yaliyofanyika katika baadhi ya vipengele vya Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298 na Kanuni zake za mwaka 2003.

Ni ukweli usiopingika kuwa, Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali inayotolewa na Serikali kupitia Wizara ninayoingoza mimi (Ofisi ya Rais- Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora).

Aidha, Serikali inatambua uwepo wa changamoto nyingi kwa baadhi ya Maafisa Watekelezaji *(Action Officers)* katika kusimamia na kutekeleza kwa usahihi Sheria, Kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya Serikali, hali inayosababisha wakati mwingine kuiingiza Serikali katika migogoro inayosababishwa na maamuzi ambayo hayakuzingatia taratibu kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Utumishi wa Umma.

Ndugu Mkuu wa Chuo, **Washiriki wa Mafunzo na Viongozi Mliopo,**
Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilianzishwa na Serikali mwaka 2000 kwa lengo la kusaidia zoezi zima la maboresho katika Utumishi wa Umma nchini yakiwemo mafunzo ya aina hii. Kwa mantiki hiyo, Serikali haina shaka na utendaji, uzoefu na weledi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania katika kutoa mafunzo kama haya. Hivyo basi Washiriki wote mliopo hapa kwa kushirikiana na waelekezi wenu hii ni fursa muafaka kwenu kuchambua na kuzielewa vizuri Sheria, Kanuni na miongozo ili muweze kuzitumia kwa usahihi wakati wa utekelezaji wa majukumu yenu ya kila siku.

Nathubutu kusema kuwa, jitihada hizi zinazofanywa na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania za kuhakikisha kwamba Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma inafafanuliwa ili itumike kwa usahihi. Katika kuhakikisha dhana ya Utawala Bora ndani ya Serikali inasimamiwa kikamilifu, imekuwa ni dhamira thabiti ya Serikali kuhakikisha kwamba Taasisi zote za Umma nchini zinafanya kazi kwa kuzingatia Sheria na Miongozo iliyowekwa na Serikali.

Ndugu Washiriki,
Nyie ni Viongozi, thamani na heshima ya Kiongozi kwa anaowaongoza ipo katika uwezo wake katika kupambanua mambo kimkakati, kuwaelewesha na kuwajengea hamasa anaowaongoza ili kufikia malengo waliyojiwekea. Kiongozi awaye yote anapenda kuendelea kutunza hadhi, heshima na thamani yake kwa anaowaongoza na jamii kwa ujumla. Jambo hili haliwezekani kama utakuwa "*Kiongozi Kilaza"* katika eneo lako la kazi.

Kama mnavyofahamu, dunia ya sasa na mifumo yake inabadilika kwa kasi kubwa. Mara nyingi kwa sisi Viongozi ni vigumu kujua jinsi ya kuendelea kuwasaidia tunaowaongoza kukabiliana na

kasi ya mabadiliko hayo pasipo sisi wenyewe kuwa na uelewa wa kutosha na mpana kuliko wao. Baadhi yetu tumejikuta tukiingizwa pabaya na kufanya maamuzi ambayo baadaye yanatufedhehesha kutokana na matokeo yake. Hii yote inachangiwa kwa kiasi kikubwa na kuwa na uelewa mdogo kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Serikali. Ndio maana leo tumewaita ili tuwekane sawa.

Ndugu Washiriki,

Mwanazuoni mmoja wa Marekani ajulikanye kwa jina la Lorna Danatone aliwahi kusema kwamba, nanukuu ***"The Key to Relevant Leadership is Continuous Learning"*** mwisho wa kunukuu. Ninatambua kwamba nyie sio wageni katika Utumishi ndani ya Serikali, lakini mkubaliane nami kwamba tunauelewa tofauti tofauti kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Serikali. Ili kuweza kujenga uelewa wa pamoja na kushughulika na changamoto tunazokutana nazo kwa viwango sawa, hatuna budi kurudi darasani na kukumbushana na kujengeana uwezo mara kwa mara. Ndio maana leo tuko hapa, ili tufundane sisi kwa sisi na tutaendelea kufanya hivyo kila inapobidi ili kuepuka migongano kati yetu, yaani kusiwe na *'double standards'* katika kutafsiri na kutekeleza miongozo tuliyonayo miongoni mwetu.

Ndugu zangu, kujenga dhana ya Uongozi wenye heshima na thamani mbele ya unaowaongoza kuna gharama yake. Wala haimaanishi kwamba uwe mtaalam katika kila eneo au katika kila wazo jipya au dhana mpya. La hasha, unachohitaji ni kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu sekta unayoisimamia na namna sekta kama yako inavyokwenda mahala pengine *(kujua wengine katika sekta kama yako huko kwingineko wanafanyeje?),* ndipo uweze kuyatafsiri mawazo hayo na kuwasiliana na unaowaongoza kwa lugha nyepesi na njia ambayo wanaweza kuielewa kirahisi ili nyote kwa pamoja muyafikie malengo yenu. Huo ndio Uongozi tunaoutarajia kutoka kwenu baada ya kutoka hapa.

Ndugu Washiriki,

Mafunzo haya ni moja ya utekelezaji wa misingi ya utawala bora unaozingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika Usimamizi na Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi. Kwa namna ya pekee nawapongeza washiriki wote wa mafunzo haya kwa kuhudhuria, licha ya changamoto za mifumo ya kiutawala katika Halmashauri zenu.

Wakati tukiwapongeza washiriki napenda kuchukua fursa hii kukishukuru Chuo cha Utumishi wa Umma kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya kwa niaba ya Serikali kuhakikisha wanaratibu

shughuli za mafunzo, utoaji wa ushauri wa kitaalamu na ufanyaji wa tafiti tumizi katika nyanja mbalimbali kwenye Utumishi wa Umma.

Nimeona niyaseme haya mbele yenu ili kuwafumbua macho juu ya nini chuo chetu kinafanya ili nanyi muone ni kwa namna gani mnaweza kukitumia Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania katika kupata majawabu ya changamoto mnazokutana nazo katika maeneo yenu ya kazi kupitia huduma za tafiti na mafunzo zinazotolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania.

Ndugu washiriki,
Serikali inamatarajio makubwa sana na mafunzo haya maalum kwenu kwa kuwa ndio kiini cha Utendaji kazi thabiti katika Halmashauri zetu. Pia, ni matarajio yangu kuwa siku zote mtazingatia misingi ya sheria za Utumishi wa Umma na Kanuni zake, mtafanya maamuzi kwa kuzingatia Taratibu na Miongozo ya Serikali ili kuepuka kuiingiza Serikali katika migogoro na gharama zisizokuwa za lazima kwa kufanya maamuzi yasiyokuwa sahihi.

Ndugu Washiriki,
Kwa kuwa ninyi ni Viongozi katika Halmashauri zenu, baada ya mafunzo haya mafupi ya siku tatu mtakwenda kuzisimamia Sheria, Kanuni, Miongozo inayotolewa na Serikali na kuitekeleza kwa Usahihi kama mtakavyokuwa mmeelekezwa na waelekezi wenu. Mtatumia weledi wenu kwa uadilifu katika kutekeleza majukumu yenu kikamilifu kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia utumishi wa umma.

Ndugu Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Idara,
Kwa kuwa leo tumekutana napenda kuzungumza nanyi baadhi ya masuala yanayoendelea huko maofisini kwenu. Kuna hili suala la uhakiki wa vyeti; Kufuatia zoezi la uhakiki wa vyeti ambalo tumekuwa tukilitekeleza, kumekuwepo na changamoto kadha wa kadha ambazo kama watendaji mmekuwa mkikutana nazo. Serikali baada ya kubaini hali hiyo, mnamo tarehe 09 Aprili, 2018 nilitoa Kauli kwa niaba ya Serikali Bungeni ili kutolea majibu changamoto hizo. Kauli hiyo ilibainisha nani **anapaswa kubakia** katika Utumishi wa Umma na nani **hapaswi kubakia**. Maelekezo ya Serikali ni kwamba **Watumishi wa makundi yafuatayo kama waliondolewa, Warejeshwe kazini mara moja, walipwe mishahara yao kwa kipindi chote ambacho walikuwa wameondolewa kazini na waendelee na ajira zao hadi watakapostaafu kwa mujibu wa Sheria**;

a) Watumishi wote ambao walikuwa na **Ajira za Kudumu au Ajira za Mikataba (Kwa Watendaji wa Vijiji na Mitaa) au Ajira za Muda *(Employment on Temporary Terms)***

ambao walikuwa kazini kabla ya tarehe 20 Mei, 2004 ulipoanza kutumika Waraka wa Utumishi *(Establishment Circular)* Na. 1 wa Mwaka 2004.

b) Watumishi wa Umma Elfu Moja Mia Tatu Sabini **(1,370)** waliolegezewa Masharti ya Sifa za Muundo kupitia Barua ya Katibu Mkuu Utumishi yenye Kumb. Na. CCB.271/431/01/P/13 ya tarehe 30 Juni, 2011.

Uamuzi huu haukuwahusu Watumishi wafuatao;

i. Watumishi ambao walikuwepo katika ajira kabla ya tarehe **20 Mei, 2004** ambao katika kumbukumbu zao rasmi kama vile taarifa binafsi ***(Personal Records)***, fomu za tathmini ya utendaji kazi ***(OPRAS)*** n.k walijaza taarifa za uwongo kwamba wanayo elimu ya kidato cha nne lakini wakashindwa kuthibitisha kwa kuwasilisha vielelezo vya sifa hizo kwa mujibu wa Miundo yao ya Utumishi;

ii. Watumishi waliowasilisha vyeti vya kughushi katika kumbukumbu za ajira yao; na

iii. Watumishi walioajiriwa baada ya **Tarehe 20 Mei, 2004** wakiwa hawana sifa ya kufaulu mtihani wa kidato cha nne kwa kuwa walijipatia ajira kinyume cha maelekezo ya Serikali.

Cha kushangaza pamoja na kwamba Maelekezo ya Serikali mnayo lakini bado tumekuwa tukipokea Watumishi kule Dodoma wakilalamikia masuala hayahaya. Waajiri na Maafisa Utumishi mpo, hii haipendezi! Timizeni wajibu wenu, wasikilizeni na kuwahudumia watumishi hukohuko kwenye Halmashauri zenu. Nimearifiwa kwamba kuna baadhi yenu mnakataa kuonana na Watumishi wanaofika kupata huduma. Jambo hili halipendezi na ninsingependa liendelee.

Ndugu Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Idara,

Suala lingine ambalo ningependa kulitolea maelekezo kwa mara nyingine tena ni kuhusu Uhamisho wa Watumishi. Naamini nyote mnatambua kwamba, uhamisho wa Watumishi unalenga kuimarisha utendaji katika Utumishi wa Umma, Serikali imekuwa ikihamisha watumishi wa Umma katika maeneo mbalimbali pamoja na kukubali maombi ya uhamisho kutoka kwa Watumishi na Waajiri kwa lengo la kuwawezesha watumishi kuhamia katika vituo vipya vya kazi. Uhamisho huo hufanyika kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali. Kwa mujibu wa miongozo hiyo ni sharti kuwepo na ridhaa ya mwajiri, nafasi wazi ya kujazwa katika kituo kipya na bajeti ya kugharamia uhamisho. Aidha, mtumishi anayeomba kuhama anapaswa kuwa amethibitishwa kazini na ametumikia katika kituo hicho kwa muda usiopungua miaka mitatu.

Kwa kuwa uhamisho wa watumishi wa Umma unaambatana na stahili za kuwezesha uhamisho huo zinazotambuliwa kisheria, ni rai ya Serikali kama ambavyo Rais wetu mpendwa *Dkt.* John Pombe Magufuli amekua akielekeza na kusisitiza mara kwa mara kwamba mtumishi asihamishwe bila kulipwa stahili zake. Stahili hizi ni kwa ajili ya kumwezesha mtumishi kutekeleza uhamisho unaofanywa bila ya matakwa yake pamoja na kufidia usumbufu unaotokea katika kufungasha mizigo na kusafirisha familia yake. Na kwa kuwa hatutaki kuongeza limbikizo la madeni, na mimi naomba nikazie hapohapo, Waajiri msiwahamishe wala kuwaombea uhamisho watumishi bila kuwa na uhakika wa fedha za kugharamia uhamisho huo. Na iwapo mtumishi atakuletea maombi ya kuhamishwa, basi katika maombi yake ni sharti athibitishe utayari wa kujigharamia kama ilivyofafanuliwa katika Kanuni L.8 ya Kanuni za Kudumu katika Utumishi wa Umma za Mwaka 2009;

Ndugu Wakurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Idara,

Pamoja na Ofisi yangu kuendelea kuelimisha na kuwakumbusha waajiri kuhusu wajibu wenu katika kusimamia utaratibu wa uhamisho wa watumishi, kumekuwepo na malalamiko na manung'uniko ya kwamba baadhi yenu mnapoletewa barua hususani za kuomba uhamisho ili mzipitishe mnakataa kupitisha. Jambo hilo ni uonevu na si sahihi, tunaposema Waajiri mpitishe hizo barua maana yake ni rahisi sana, mwenye Mamlaka ya kutoa ridhaa mtumishi huyu ahame au asihame ni yule anayendikiwa, wewe kama mwajiri jukumu lako ni kupitisha na kutoa maoni yako kuhusu ombi hilo ili mwenye Mamlaka akafanye uamuzi na si vinginevyo. Rai yangu kwenu ni kuwataka kutumia vizuri fursa hiyo kuweka maoni yanayoonesha picha halisi ya watumishi ili kutoathiri utendaji kazi baada ya watumishi hao kuhama. Naomba kuwatoa shaka na kuwahakikishia kwamba maoni yenu yanazingatiwa. Mara zote tumekuwa tukitoa msisitizo kwa Mamlaka za uhamisho kuhakikisha kwamba, uhamisho unaofanywa unazingatia maoni yanayotolewa na Waajiri pamoja na haki ya mtumishi bila kuathiri maslahi ya umma.

Katika eneo hili la uhamisho, napenda pia kutoa angalizo. Wapo watumishi wanaoajiriwa katika maeneo yenye upungufu mkubwa wa watumishi ambao wakishaajiriwa tu wanaanza kuomba uhamisho. Naomba ifahamike kuwa kuajiriwa kwao kulilenga kuwezesha wananchi wa maeneo hayo kupata huduma muhimu na si vinginevyo. Hivyo wasichukulie maeneo hayo kuwa ni ya kujipatia ajira na ndani ya muda mfupi kuomba kuhama na kuacha wananchi bila huduma.

Hata hivyo ninatambua yapo maeneo mengine ambayo ni ya pembezoni na yenye mazingira magumu. Rai yangu kwenu waajiri, tumieni mamlaka mliyokasimiwa kuhakikisha kwamba Watumishi wanapata fursa ya kubadilishana vituo vya kazi hususani ndani ya Halmashauri au

Mkoa husika pale inapowezekana ili kuwapatia fursa ya kubadili mazingira ya kazi na kuwamotisha watumishi walio katika maeneo yenu ya usimamizi.

Ndugu Washiriki,

Serikali yetu katika Awamu zote tano imekuwa na utaratibu wa kuweka kila jambo katika kumbukumbu. Toka enzi na enzi taarifa rasmi za Serikali huwekwa kwenye maandishi hata kama awali ilitolewa kwa mdomo. Mawasiliano, maelekezo na maamuzi yote ndani ya Serikali yamekuwa yakifanyika kwa njia ya maandishi. Ndiyo maana tunasema *'Government Moves on Paper'* Ni muhimu sana tukalizingatia hili ili kutoathiri utendaji wa kazi wetu na kutunza Utamaduni tuliokwishajiwekea.

Sambamba na hilo, siku za hivi karibuni kumejitokeza utamaduni ndani ya Utumishi wa Umma ambao si mzuri na nisingependa uendelee. Kumekuwa na tabia ya baadhi yenu kutojibu barua, tabia hii inakera, inakwamisha shughuli za Serikali na kuwakwaza sana wananchi na wadau wengine tunaowahudumia. Kwa wale waliomsikia Mheshimiwa Rais jana wakati akimwapisha Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ameonesha kukereka na utamaduni huo wa kutojibu barua. Naamini nyote mnayo mikataba ya huduma kwa mteja katika Halmashauri zenu. Mnapotoa huduma izingatieni hiyo maana ndiyo mkataba uliopo kati yako na mteja wako, kinyume na hapo lazima utalalamikiwa tu. Inakugharimu nini kujibu barua?
Hakuna ubishi kwamba zipo baadhi ya barua zinazohitaji uchambuzi wa kina na kufanya mashauriano na mamlaka zingine, jambo ambalo linaweza kuhitaji muda mwingi. Hata kama unalishughulikia suala lililoletwa kwako, basi mjulishe mhusika kwamba barua yako nimeipokea, ninaifanyia kazi. Hii itakujengea heshima na thamani kwa unaowahudumia.

Ndugu washiriki;

Zaidi ya asilimia 75 ya muda wetu tunautumia makazini kwetu, huu ndio ukweli. Mazingira haya ya ofisi zetu yanatuhifadhi sisi pamoja na wateja wetu wanaofika kupata huduma. Cha kushangaza, baadhi yetu tunazembea katika kuyatunza mazingira haya yanayotuhifadhi kwa muda wote huo. Katika baadhi ya Ofisi za umma, imekuwa kawaida kukuta mazingira ya ofisi yakiwa machafu, mathalani maeneo ya maliwato, wengi mtakuwa mashahidi wangu kwamba maeneo haya yanasahaulika sana. Mtu ni afya, pamoja na kuwa na shughuli nyingi nawakumbusha kuyaangalia mazingira ya ofisi zetu. Kwani kupitia mazingira yanayotuzunguka, wateja wetu wanatutathimini na kupima ustaarabu wetu.
Pia yapo mambo mengine madogomadogo tunayasahau hii haipendezi, mfano unafika kwenye ofisi ya Serikali unakuta Bendera ya Taifa ambayo ni moja ya utambulisho wa Nchi yetu

imechanika na kuharibika kabisa lakini bado inapeperushwa, hii ni aibu na sintapenda kuiona huko kwenu, Serikali yetu haijafikia umasikini wa kushindwa kununua bendera. Kama Mkurugenzi unakosa Sh. 80,000 ya kununua bendera ya ofisi katika mafungu yako inabidi ujitafakari kama kweli unatosha.

Ndugu Mkuu wa Chuo,

Kabla sijahitimisha hotuba yangu leo, napenda kutumia fursa hii kutoa wito kwamba mara baada ya kumaliza kutoa mafunzo haya katika taasisi zilizo chini ya TAMISEMI, itapendeza sana kama Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kitaandaa mafunzo kama haya kwa ajili ya Wakuu wa Taasisi zote za Umma nchini -upande wa Serikali Kuu, ili nao waweze kuhudhuria mafunzo haya muhimu. Naomba niwahakikishie kwamba Ofisi yangu itakuwa tayari kabisa kushirikiana nanyi pale itakapobidi.

Ndugu Mkuu wa Chuo na Washiriki,

Mwisho kabisa, lakini si mwisho kwa umuhimu niwakumbusheni kuhusu uzingatiaji wa Maadili ya Utumishi wa Umma kama Viongozi. Kiongozi unapaswa kuwa mfano kwa tabia njema, kupinga rushwa na kuzingatia maadili ya Uongozi kwa ujumla. Rushwa ni adui wa haki, ukiwa Kiongozi jukumu lako kubwa ni kusimamia haki. Lakini usipojiepusha na rushwa huwezi kutenda haki kwa unaowaongoza na zaidi sana utaishia kuhujumu rasilimali za nchi. Wewe utakua msaliti miongoni mwetu, hauna tofauti na abiria anayetoboa mtumbwi katikati ya safari, hatuwezi kukuvumilia ni lazima tukutose majini ili tuendelee na safari na kuweza kufika salama huko tuendako.

Katika maeneo yenu ya kazi, limekuwa jambo la kawaida kukuta baadhi yenu au madiwani kwa waziwazi au kwa kificho kupitia makampuni yenu, mmekuwa mkifanya biashara na Halmashauri zenu. Jambo hili limepelekea kuwepo kwa mgongano wa maslahi na kuisababishia Serikali hasara kubwa. Huwezi kuwa hakimu wa kesi yako mwenyewe na bado ukatenda haki. Nyie wenyewe mnashiriki kwenye vikao vya tenda, nyie wenyewe mnataka kupewa tenda, haki itatendeka hapo kweli? Haiwezekani!

Huenda mnayafanya haya kwa makusudi au kwa sababu ya kukosa uelewa. Kwa sehemu kubwa tabia hii inachangiwa na kutotelekeza miongozo na maelekezo mbalimbali yanayotolewa mara kwa mara na Serikali. Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwishatoa maelekezo ya kuwataka waajiri wote kuwaalika TAKUKURU na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kila mnapokuwa na mkusanyiko wa Watumishi katika maeneo yenu ya kazi ili waweze kutoa mada.

Iwe Baraza la Madiwani, Baraza la Wafanyakazi au mikutano mingine mnapaswa kuwaalika wataalamu hawa ili wawapeni elimu kuhusu mapambano dhidi ya rushwa na uzingatiaji wa maadili katika utekelezaji wa majukumu yenu ya kila siku. Tafadhali lizingatieni hilo na pendeni kujielimisha mara kwa mara ili kuendana na kasi ya Awamu ya Tano.

Kazi kubwa niliyopewa kwa siku ya leo ni kufungua mafunzo haya maalumu kwa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara za Utawala na Rasilimaliwatu wa Halmashauri nchini. Lakini kabla ya kumalizia hotuba yangu napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa maandalizi mazuri ya mafunzo haya, na ninawashukuru wote mlioshiriki kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha shughuli hii ya ufunguzi wa mafunzo haya.
Baada ya kusema hayo, sasa ninayo heshima kubwa kutamka kwamba,

“**MAFUNZO MAALUM KUHUSU UTEKELEZAJI SAHIHI WA SHERIA, KANUNI, TARATIBU NA MIONGOZO KATIKA UENDESHAJI WA UTUMISHI WA UMMA KWA WAKURUGENZI WA HALMASHAURI NA WAKUU WA IDARA ZA UTAWALA NA RASILIMALIWATU” NIMEYAFUNGUA RASMI LEO TAREHE 01 OKTOBA, 2018**.

Asanteni kwa kunisikiliza.